BUKU LA 25

Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb,

Natumai kuwa ulikuwa na wiki nzuri na unajiandaa kuwa na wikendi salama na ya kupumzika. Kama wilaya ya shule, tunayo furaha kwamba viashiria vyote vinaendelea kulingana na maandalizi yetu ya chaguo la mafunzo ya ana kwa ana kwa wanafunzi na familia ambazo zinavutiwa. Tunatambua pia kuwa kuna familia na wafanyakazi ambao walionyesha wasiwasi wakati wa mkutano wa Bodi mnamo Februari 11 na siku zilizofuata. Tumetumia siku hizi chache zilizopita kushughulikia matatizo yaliyotambuliwa na tumetoa sasisho hapa chini.

Nimefurahishwa sana na timu yetu ambayo imefanya kazi bila kuchoka katika miezi michache iliyopita. Ninajivunia wilaya yetu na hadithi ya kweli ya mabingwa waliojitolea kwa maono yetu ya Wahitimu wa Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb, hata katikati mwa janga. Tutaendelea kufanikiwa pamoja.

Ninatazamia tukio letu la Hali ya Wilaya lenye mada ya “Kuinua uzoefu wa DCSD hadi kiwango kipya cha ubora” mnamo Februari 23 na kushiriki mipango yetu kwa kipindi kilichosalia cha mwaka cha masomo.

Kamati ya Ushauri wa Wanafunzi

Nilikuwa na wakati mzuri na Kamati yetu ya Ushauri wa Wanafunzi wiki hii iliyopita. Wanafunzi walijadili hisia zao kuhusu mazingira ya mafunzo ya mtandaoni, jinsi janga hilo limewaathiri kimasomo na kijamii, na kile ninachopaswa kuzingatia wakati wa kupanga wanafunzi kurudi. Nilithamini sana maoni na majibu yao ya busara. Najivunia sana wanafunzi wetu. Asante kwa kuwa mifano na viongozi bora kwa wanafunzi.

Reach Georgia

Nashukuru mshirika wetu Reach Georgia kwa kuwa na siku nzuri ya kutia saini. Wanafunzi wanne wa DCSD walipokea $10,000 kila mmoja na ushirikiano huu unatoa ufikiaji mkubwa wa vyuo vikuu kwa wanafunzi wetu na kuwaandaa kwa ajili ya Mahali pa Kazi katika Karne ya 21. Asante kwa kujitolea kwako kwa wanafunzi wetu!

Siku ya Kuwa Nje

Ninafurahiya kushiriki kwamba tulikuwa na Siku yenye mafanikio ya kuwa nje mtandaoni katika Mkoa wa VI. Niliona mkutano wa timu ya hisabati ya darasa la nne

ulioshirikiana sana katika Shule ya Msingi ya Peachcrest na mkutano wa uboreshaji unaoendelea katika Shule Mbadala ya DeKalb. Ningependa kuwashukuru wakuu na wafanyakazi wa shule hizo kwa kunikaribisha na kwa bidii na kujitolea kwao.

Mpango Kamili Mkuu - Mkutano wa Ukumbi wa Jiji #1

Tafadhali jiunge nasi mnamo Februari 25 kutoka saa 6 - 7:30 ambapo wakati timu itakua na Mpango Kamili Mkuu (CMP). Mkutano utatoa muhtasari wa mchakato wa kupanga, jinsi unaweza kushiriki, na cha kutarajia katika miezi ijayo.

Maswali kwa timu yanaweza kuwasilishwa mapema kwenye anwani hii ya barua pepe: CMP@dekalbschoolsga.org

Mkutano unaweza kufikiwa hapa.

Hali ya Wilaya

Nitatoa hotuba ya Hali ya Wilaya mnamo Februari 23, 2021. Mpango huu utakuwa “sherehe ya ndani ya gari” katika maegesho ya magari yaliyo 4550 Greer Circle kule Stone Mountain. Maegesho hayo ya magari yatafunguliwa saa 4:15 p.m. na mpango utaanza saa 5:30 p.m. Ninafuraha kushiriki jinsi tunavyoboresha uzoefu wa DCSD hadi kiwango kipya cha ubora. Angalia mwaliko wetu hapa.

Mwongozo wa CDC

Kama nilivyosema hapo awali, tumekuwa thabiti katika njia yetu ya kuongozwa na sayansi na mwongozo kutoka kwa Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC). Kulingana na mwongozo wa hivi karibuni kutoka kwa CDC, Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb (DCSD) iko kwenye njia sahihi ya kuwakaribisha wanafunzi wetu kurudi salama katika majengo ya shule na viwango vyetu vya utayari wa majengo na kutekeleza mikakati ya kupunguza.

Usalama wa wafanyakazi na wanafunzi wetu unaendelea kuwa kipaumbele chetu cha kwanza. CDC inapendekeza kwamba mikakati ifuatayo ya kupunguza itekelezwe ili kupunguza hatari ya maambukizo ndani ya shule. Hivi ndivyo DCSD inavyoweka jamii yetu salama:

1. Vaa barakoa wakati wote na inavyofaa. Barakoa zinapaswa kufunika kabisa pua na mdomo na kutoshea vyema pande zote za uso bila nafasi wazi. Kinga ya uso haipaswi kuchukua nafasi ya barakoa.

2. Kujitenga na watu – Unda mazingira salama kwa kujizoeza kujitenga na watu kwa angalau futi 6 kati ya watu. DCSD pia inapanga vikundi vya watu, ambayo inajumuisha kupanga wanafunzi, na wakati mwingine wafanyakazi, kukaa pamoja wakati wote wa siku ya shule ili kupunguza maambukizo. Ratiba za nyakati tofauti kama vile saa za kuwasili na kuchukuliwa na maeneo kulingana na kikundi pamoja na kupunguza wageni na shughuli ambazo sio muhimu pia zitatekelezwa.

3. Nawa mikono yako - Nawa mikono ukitumia sabuni na maji kwa angalau sekunde 20 na epuka kugusa uso. Jifunike unapokohoa na kupiga chafya kwa kitambaa wakati hujavaa barakoa na nawa mikono mara baada ya kupenga kamasi, kukohoa, au kupiga chafya.

4. Safisha na utakase – kanuni msingi ya CDC ya kusafisha na kudumisha vifaa vyenye afya ni kusafisha mara kwa mara maeneo yanayoguswa sana (kama vile virungu vya mlango na soketi za umeme). DCSD inatoa vifaa vya kutosha (kwa mfano, sabuni, taulo za karatasi, kieuzi cha mkono chenye angalau asilimia 60 ya kileo, vipangusio vya kuua viini, barakoa) ili kuhakikisha usalama. Hapa kuna hatua nyingine za DCSD za kuwa salama:

    - Kusafisha maeneo yanayoguswa mara kwa mara
    - Kubadilisha mipangilio ya darasa
    - Kuweka vizuizi vya mwili na ishara ya COVID-19
    - Kuzuia vifaa vinavyotumiwa na wengi

5. Utafutaji wa watu waliokaribiana - DCSD huendelea kushirikiana na Idara ya Afya ya Umma ya Georgia na Bodi ya Afya ya DeKalb ambayo huwatambua watu ambao wametangamana kwa karibu hivi karibuni na mtu (watu) walioambukizwa COVID-19 ili kuzuia kuenea zaidi. Ufuatiliaji wa watu waliokaribiana husaidia kupunguza COVID-19 kuenea kwa:

    - Kuwajulisha watu wanaweza kuwa wameambukizwa COVID-19 na wanapaswa kufuatilia afya yao ili kuchuguza ishara na dalili za COVID-19.
    - Kuwasaidia watu ambao wanaweza kuwa wameambukizwa COVID-19 wapimwe.
    - Kuwaomba watu wajitenge ikiwa wana COVID-19 au kujiweka karantini ikiwa wamekaribiana na mtu.

6. Mfumo wa kupitisha hewa katika majengo – DCSD hufuatilia mara kwa mara nyumba za shule na vituo ili kuona kuwa vina mfumo sahihi wa kupitisha hewa. Tumeongezea mfumo wa kupitisha hewa na uchujaji katika vitengo vyetu vya HVAC ili kufikia mwongozo wa CDC na tasnia kwa kadri inayowezekana katika kila moja ya vitengo vyetu.

Mikakati ifuatayo ya shule ya DCSD kuwa tayari pia imewekwa ili kuweka DCSD salama:

7. Chanjo - Wauguzi 31 wa DCSD wamefundishwa kutoa chanjo kwa watu binafsi mara tu chanjo itapatikana kwa Daraja 1B, ambayo inajumuisha walimu wetu. DCSD iko tayari kufuata mpango wa utekelezaji wa chanjo ya COVID-19 huko Georgia.

8. Kupima – DCSD inafurahia kufanya kazi na wachuuzi ili kupima COVID -19 kwa wanafunzi, wafanyakazi, na familia. Upimaji unaweza kusaidia watu kuamua ikiwa wanafunzi, wafanyakazi na familia wameambukizwa SARS-CoV-2 – haijalishi kama wanaonyesha dalili na kama wamo katika hatari ya kueneza maambukizo kwa wengine.

9. Barakoa za uso zimeagizwa kwa wafanyakazi wote.

10. Walimu wote wakuu watapokea mgao unaofaa wa Msaada wa kununua PPE za ziada iliyoombwa na wafanyakazi.

11. Agizo letu la teknolojia mpya limewasilishwa na tunatarajia vifaa vyetu vipya ndani ya mwezi ujao. Kamera za wavuti zimesambazwa kwa shule zote. Kuanzia Jumatatu, Februari 22, tutakuwa tukifanya tathmini maalum za utayari wa teknolojia ili kushughulikia matatizo yoyote yaliyopo.

Tafadhali endeleeni kujijali, kuwa waangalifu wenyewe kwa wenye, na muhimizwe kwamba kwa pamoja tutaunda DCSD yenye nguvu.

Wako mwaminifu,

Bi. Cheryl Watson-Harris